# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL 4
# KISWAHILI PAPER 2 QUESTIONS

**1. UFAHAMU (Alama 15 )**

**Soma Makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia**

**1. Licha ya kuwa na historia ya kiasi, maisha ya binadamu ni kioja kikubwa.**

**Hebu jiulize jinsi uhai wako mwenyewe ulivyoanza sembuse unavyoweza**

**kupumua na kuishi siku nenda siku rudi. Dini zimefahamisha kuwa sisi binadamu**

**tumeumbwa na Mwenyezi Mungu Muumba. Hata hivyo Muumba hutumia mume na**

**mke kutuanzishia maisha yetu humu duniani. Uhai wa hapa duniani huanzia katika tumbo la**

**mwanamke muda mfupi tu baada ya mume na mke kushirikiana katikau tendo la kujamiana.**

**Katika ngono hii yenye ufanisi, mbegu moja ya manii kutoka kwa mwanamume hudunga na**

**kujiingiza katika yai la mwanamke huku ikilirutubisha. Tangu hapo, mtu huwa na mama akawa mja**

**mzito. Hatua ya kwanza ya yai!**

**Wanasayansi wametuthIbitishia kuwa mbegu katika shahawa kutoka kwa mwanamume**

**na kromosomu ishirini na tatu nalo yai la mwanamke lina idadi iyo hiyo ya kromosomu.**

**Basi katika hatua ya kwanza ya uhai wake, binadamu ana kromosomu arubaini na sita.**

**Kromosomu hizo zote ndizo humfanya mtu kuwa mkamilifu na kukadiria mambo mbalimbali**

**adhimu.**

**Kwa mfano. Hukadiria kama kiumbe kitakuwa cha kike au cha kiume, mtu mweupe au mtu**

**mweusi,**

**mwerevu au wa akili chache, mwenye nywele za singa au kipilipili, atakuwa na damu ya namna**

**gani,**

**michoro ya vidole vyake itakuwa vipi na hata utu wake utakuwa wa namna gani katika siku za**

**usoni.**

**Elimu yote anayopata mtu kutoka kwa jamii na mazingira huweza tu kujenga juu ya**

**yaliyokwisha kuanzilishwa na kromosomu katika yai lililorutubishwa tumboni. Haihalisi kabisa**

**kufikiria kwamba katika hatua za mwanzo tumboni mwa mama, kiumbe huwa katika hali ya ukupe.**

**La hasha! Yeye hujitegemea kwa vyovyote na upekee wake.Hatangamani na mama yake.**

**Roho yake humdunda mwenyewe na damu yake ambayo huenda ikawa tofauti kabisa**

**na mama yake, humtembeau na kumpiga mishipani mwake. Isitoshe, yeye si mojawapo**

**katika viungo vya mwili wa mama yake vinavyodhibiti katika himaya yake ndogo.**

**Amini usiamini, hapana binadamu hata mmoja ambaye amewahi kuwa sawa**

**kimaumbile na mwingine na wale watakuwepo. Hata watoto pacha kutoka yai**

**moja la mama hawawi sawa; lazima wahitilafiane. Si nadra kusikia mtu amepata ajali**

**akahitaji msaada wa damu na pakosekane kabisa mtu hata mmoja kutoka jamaa yake wa kumwauni.**

**Basi ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni**

**MASWALI**

**a) Kwa nini mwandishi anadai kuwa maisha ya binadamu ni kioja kikubwa? (alama 2)**

**……………………………………………………………………………………..**

**……………………………………………………………………………………..**

**b) Kwa mujibu wa taarifa hii,ni nini maana ya "ngono yenye ufanisi?" (alama 2)**

**……………………………………………………………………………………..**

**……………………………………………………………………………………..**

**c) Uchunguzi wa sayansi umekita mizizi imani gani ya kidini? (alama 2)**

**……………………………………………………………………………………..**

**……………………………………………………………………………………..**

**d) Kwa mujibu wa makala haya, thibitisha kuwa kiumbe kilicho tumboni mwa mamake hakiko**

**katika "hali ya ukupe." (alama 4)**

**……………………………………………………………………………………..**

**……………………………………………………………………………………..**

**……………………………………………………………………………………..**

**……………………………………………………………………………………..**

**e) Toa sababu ya elimu ya kutoka kwa jamii na mazingira kuelekea kuwa bure ghali. (alama 1)**

**……………………………………………………………………………………..**

**……………………………………………………………………………………..**

**f) …"hapana binadamu hata mmoja ambaye amewahi kuwa sawa na mwingine…"**

**kulingana na makala haya eleza sababu za hali hii. (alama 2)**

**……………………………………………………………………………………..**

**……………………………………………………………………………………..**

**……………………………………………………………………………………..**

**…………………………………………………………………………………………..**

**g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. (alama 2)**

**i) Himaya**

**…………………………………………………………………………………………..**

**…………………………………………………………………………………………..**

**ii) kumwauni**

**…………………………………………………………………………………………..**

**…………………………………………………………………………………………..**

**2. MUHTASARI: (Alama 15 )**

**2. Biashara ya kimataifa ni muhimu sana katika ukuaji wa nchi yoyote ile.**

**Nchi mbalimbali zimekuwa zikitegemeana kwa namna moja au nyingine.**

**Kwa mfano, nchi ya Kenya imekuwa ikiuza maua na mboga katika nchi za ng'ambo na kupata**

**fedha za kigeni ambazo hutumiwa humu nchini kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.**

**Biasha ya kimataifa huziwezesha nchi ambazo hasizalishi bidhaa hizo kutoka nch**

**i nyingine inayohusiana nayo kibiashara. Mathalan, Kenya ni nchi ambayo imekuwa**

**ikitegemea kilimo lakini haijaendelea katika sekta ya viwanda. Kenys huagiza bidhaa**

**kama vile vipuri vya magari na hata magari yenyewe kutoka nchi kama vile Japani.**

**Nayo Kenya huuza mazao ya shambani kama vile pareto, chai na kahawa ng'ambo.**

**Kupitia kwa biashara ya kimataifa, nchi hupata masoko kwa bidhaa zake,**

**kwa vile biashara ya kimataifa huziwezesha nchi husika kuzalisha kiasi kikubwa cha**

**bidhaa kuliko mahitaji yake ya nyumbani. Nchi basi hulazimika kutafuta masoko nje ya**

**mipaka yake. Kwa njia hii uchumi wa nchi huendelea kuimarika.**

**Aidha biashara ya kimataifa huwezesha nchi kupata huduma za kitaalauma ambazo**

**hazipatikani katika nchi husika. Kuna nyanja za kiuchumi huhitaji wataalamu mahsusi.**

**Kwa mfano, katika sekta ya matibabu nchini humu tumepata kwamba kuna baadhi ya**

**wagonjwa huagiziwa madaktari kutoka ng'ambo na hata kupelekwa ng'ambo kwa uchunguzi na**

**matibabu zaidi.**

**Biashara ya kimataifa hukuza ushirikiano wa kimataifa. Nyakati za majanga ya kimaumbile na hata**

**mengine**

**yanayosababishwa na kutowajibika kwa binadamu, nchi hupata usaidizi kutoka nchi za ng'ambo.**

**Kwa mfano wakati wa mkasa wa bomu wa 1998, Kenya ilipata msaada wa kukabiliana na janga hili**

**kutoka**

**Israel, Marekani na hata Ujerumani ambako baadhi ya waathiriwa wa mkasa huo walipelekwa kwa**

**matibabu zaidi.**

**Ushirikiano huu wa kimataifa huwezesha wananchi fulani kwenda kusomea na hata kufanya kazi**

**katika nchi nyingine.**

**Katika miaka ya hivi karibuni Wakenya wamekuwa wakienda kusomea vyuo vikuu vya ng'ambo.**

**Wengine wamediriki kupata kazi katika mashirika ya kimaitafa katika nchi mbalimbali**

**kama vile Afrika Kusini, Rwanda,Msumbiji na kadhalika.**

**Biashara ya kimataifa huleta ushirikiano wa kisasa na uelewano zaidi kati ya madola mbalimbali.**

**Mathalan muungano wa nchi za Afrika Mashariki- Kenya, Uganda na Tanzania hauchangii tu kuleta**

**maufaa ya kiuchumi bali huleta ushirikiano zaidi wa kisiasa.**

**Ingawa biashara ya kimataifa ina wateja, biashara hii huandamana na hasara mbalimbali.**

**Biashara hii imesababisha kuwepo kwa masoko huru ambayo yameleta ushidani mkubwa**

**kwa wafanyibiashara wadogoi humu nchini. Baada ya wafanyibiashara wamelazimika kufunga**

**biashara zao baada ya kufilisika. Ushuru mkubwa unaotozwa baadhi ya bidhaa zinazoingia nchini**

**huwafanya wananchi kutofaidika kwa bidhaa na huduma kutoka nje.**

**Aidha, kuna ucheleweshaji wa bidhaa zilizoagizwa. Bidhaa hizi mara nyingi huchukuwa**

**muda kabla ya kutoka nchini , kwa hivyo wafanyishiara wa kimataifa huchukuwa fursa hii**

**kulangua dawa mbalimbali za kulevya ambazo huwaathiri vijana wanchi husika.**

**Wengine huhusika katika vitendo vya kigaidi. Kama vile uchomaji wa majengo mbalimbali kwa**

**bomu na mauaji ya wananchi wasio na hatia.**

**Ni ukweli kuwa biashara ya kimataifa ina hasara zake. Hata hivyo biashara hiyo ni mhimili**

**mkubwa wa uchumi wa mataifa machanga.**

**Maswali**

**a) Fupisha aya tano za mwanzo kwa maneno 80 (alama 9,1 ya utiririko)**

**Matayarisho**

**..................................................................................................................................................**

**..................................................................................................................................................**

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

**Jibu**

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..........................................................................

**b) Fupisha aya tatu za mwisho kwa maneno 60. (alama 6,1 ya utiririko)**

**Matayarisho**

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

**Jibu**

.......................................................................................................... ..............................

.......................................................................................................... ..............................

**3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40 )**

**3. Eleza tofauti kati ya sauti zifuatazo: (alama 2)**

**a) /a/ na /t/**

………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………...

**b) Tambua viwakilishi katika sentensi hizi: (alama 2)**

**i) Cha kuvunda hakina ubani.**

…………………………………………………………………………………..

**ii) Kwake hakuingiliki**

…………………………………………………………………………………..

**c) Onyesha matumizi mawili ya koloni. (alama 2)**

…………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………..

**d) Bainisha silabi mbili funge katika neno lifuatalo: Takriban. (alama 1)**

…………………………………………………………………………………..

**e) Tunga sentensi moja ukitumia kihisishi cha masikitiko. (alama 1)**

…………………………………………………………………………………..

**f) Andika maana tatu ya sentensi hii. (alama 3)**

**Mwaliko huo ulitushtua.**

…………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………..

**……………………………………………………………………………………**

**g) Andika vitenzi hivi katika hali ya kuendesha. (alama 2)**

**i) Nawa…………………………………………………………………………**

**ii) Takata…………………………………………………………………………..**

**h) Tunga sentensi MOJA kwa kutumia vitate vifuatavyo ili kubainisha**

**maana:- (alama 2)**

**Kuna/guna.**

**……………………………………………………………………………………**

**……………………………………………………………………………………**

**i) Andika kwa ukubwa wingi (alama 2)**

**Mwizi aliiba nguo na kiti.**

**……………………………………………………………………………………**

**j) Yakinisha sentensi hii katikai nafsi ya pili umoja. (alama 2)**

**Tusipoelewana na wazazi hatutaelimishwa.**

**……………………………………………………………………………………**

**……………………………………………………………………………………**

**k) Andika visawe vya maneno yafuatayo: (alama 2)**

**i) barabara**

**……………………………………………………………………………………**

**ii) Kiuno**

**……………………………………………………………………………………**

**l) Unda nomino kutokana na vitenzi hivi: (alama 2)**

**i) Zua………………………………………………………………..**

**ii) Sakini……………………………………………………………….**

**m) Andika sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo uliyopewa: (alama 2)**

**Mama alishangilia arusi ya mwana**

**Anza: Mwana…**

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

**n) Onyesha viambishi kitenzi hiki: (alama 1)**

**Sajilika**

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

**o) Changanua sentensi hii kwa mchoro wa jedwali. (alama 4)**

**Mwalimu alimpiga mtoto ambaye alikuwa mgonjwa.**

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

**p) Geuza sentensi ifuatayo kwa msemo halisi. (alama 3)**

**Kasisi alitaka kujua kama waumini wangeenda kuhudhuria misa siku hiyo.**

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

**q) Onyesha matumizi ya 'na' katika sentensi hii (alama 3)**

**Mwongongi na Ayuma wanapendana**

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

**r) Kamilisha tashbiha hii. (alama 1)**

**Adimika kama**

**…………………………………………………………………..**

**s) Neno 'taa' linaamisha chombo cha kutoa mwangaza. Eleza maana nyingine mbili ya neno 'taa'**

**(alama 2)**

**………………………………………………………………………………….**

**………………………………………………………………………………….**

**t) Tumia kirejeshi "O" kuandika sentensi ifuatayo upya (alama 1)**

**Simiti ambayo alijengea alifaa**

**………………………………………………………………………………….**

**………………………………………………………………………………….**

**4. ISIMUJAMII (Alama 10 )**

**4. a) i) Lafudhi ni nini? (alama 1)**

**………………………………………………………………………………….**

**………………………………………………………………………………….**

**ii) Eleza sababu mbili za utokeaji wa lafudhi. (alama 2)**

**………………………………………………………………………………….**

**………………………………………………………………………………….**

**b) Huku ukitoa mifano, eleza sifa saba za sajili ya maabadani. (alama 7)**

**…………………………………………………………………………………………………………………**

**……………………………………………………………………………………………… …………………….**

**……………………………………………………………………………………………….……………………..**

**……………………………………………………………………………………………… …………………….**

**……………………………………………………………………………………………… …………………….**

**…………………………………………………………………………………………………………………**